

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA THELATHINI NA TANO**

**24 MEI, 2021**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA TANO – TAREHE 24 MEI, 2021

#### I. DUA:

#### II. KIAPO CHA UAMINIFU:

1. Mhe. Dkt. Florence George Samizi
2. Mhe. Kavejuru Eliadory Felix

#### III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

##### WAZIRI WA KILIMO:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

##### MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

#### IV. MASWALI:

##### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**283. MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE NGASSA (IGUNGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaipatia Hospitali ya Wilaya ya Igunga Gari la kubebea Wagonjwa kwa kuwa lililopo limechakaa sana.

**284. MHESHIMIWA CHARLES MUGUTA KAJEGE (MWIBARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuipunguzia mzigo TARURA kwa kuzihamishia TANROADS barabara za Bulamba – Karukekere – Nakatubai – Igunchi – Mwitende na Busambara - Mugara zilizopo katika Jimbo la Mwibara.

**285. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itakipatia Kituo cha Afya cha Muyama Wilayani Buhigwe vifaa vya *Ultrasound* na *X-ray*.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**286. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa Masoko ya Kimataifa ya Kitega Uchumi ya Murongo na Nkwenda ili kuongeza chachu ya maendeleo ya Wilaya ya Kyerwa.

**WIZARA YA MAJI:**

**287. MHESHIMIWA DEUS CLEMENT SANGU (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza maji kutoka katika Mradi wa Maji wa Kata za Miangalua na Mnokola katika Jimbo la Kwela.
- (b) Je, ni lini Serikali itapeleka pesa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi katika maeneo hayo.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**288. MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurasimisha Bandari ya Mbweni kuwa Bandari ndogo.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**289. MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA (MAKETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, upi ni mkakati wa Serikali wa kuendeleza Shamba la Mifugo la Kitulo.

**290. MHESHIMIWA RIDHIWANI JAKAYA KIKWETE (CHALINZE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni lini Serikali itapima eneo la Mifugo la Ruvu na kulikabidhi kwa Halmashauri ya Chalinze.

**WIZARA YA NISHATI:**

**291. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE (NSIMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Wananchi wa Kata ya Ugalla watapatiwa umeme wa REA III.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**292. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, Serikali ina mkakati gani dhidi ya vitendo vya ukatili vinavyofanywa kwa Wanawake na Watoto.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**293. MHESHIMIWA VINCENT PAUL MBOGO (NKASI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro kati ya Hifadhi ya Lwafi iliyopo Nkasi Kusini na Wananchi wa Vijiji vya Mlambo, King'ombe, Tundu na Kata ya Wampembe

**V. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA KILIMO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**DODOMA  
24 MEI, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**